GAZETI LA KWANZA LA ISLAM KUTOLEWA KWA LUGHA YA KISWAHILI - MWAKA 1936

AHMADIYYA MUSLIM JAMAAT TANZANIA

Mapenzi Mungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE

JUZU NO. 241 **Dh.Hijjah-M/haram** 1445/6 **AH** **Julai–** 2024 **Wafa** 1403 **HS** **BEI TSH 800/=**

Karibu Maulana Sh. Khawajja Muzaffar Ahmad. Amir na Mbashir Mkuu Jamati Tanzania Julai, 2024.



JAMAAT AHMADIYYA YAPATA MWALIKO RASIMI KUHUDHURIA KIKAO

UK. 07



Ijtimaa ya 34, Khuddam Ahmadiyya Tanzania Yafana.

UK. 05





Mjue Jinni

Sehemu ya Kwanza.
Jinni ni nikiumbe gani.?

UK. 3

Ijtimaa ya 34 ya Khuddam Ahmadiyya Tanzania Yafana >UK .05

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

KUSAMEHE KULIKO TUKUKA

Kusamehe ni khulka njema. Ni kutambua ubinadamu wako kuwa wewe hukukamilika na kuna siku nawe utalazimika kuomba msamaha na kusamehe. Hiyo ni aina moja ya kusamehe.

Lakini khulka ya kumsamehe mtu wakati una nguvu na uwezo wa kumuadhibu, hicho ndicho kiwango cha hali ya juu cha kusamehe. Kiwango hiki kilichokamilika na chenye shani na utukufu mkubwa kilioneshwa na Mtukufu Mtume Muhammad[saw]. Ni kweli ya kwamba Mtume Muhammad[saw] alikuwa na khulka njema na ametumwa kuwa rehema kwa dunia nzima.


Mtukufu Mtume Muhammad[saw] alikuwa ametoka vitani ilikuwa ni wakati wa mchana na jua lilikua kali, masahaba walitafuta kivuli na Mtukufu Mtume Muhammad[saw] akapata kivuli mbali kidogo kutoka kwa Masahaba zake. Usingizi ulimpitia na ghafla adui mmoja kwa jina la Dathur alikwenda taratibu na kuchukukua jambia ya Mtukufu Mtume Muhammad[saw] iliyokuwa juu ya Mti. Yule adui alichukua jambia lake na kusimama mbele yake huku akisema, ewe Muhammad nani anaweza kukuokoa kwa hivi sasa? Kwa sauti iliyo imara isiyokuwa na wasiwasi wowote Mtukufu Mtume[saw] alimjibu ALLAH, sauti ile yenye uhakika na nguvu kubwa ilipotoka yule adui akaanza kutetemeka mwili mzima. Katika hali hiyo ya kutetemeka jambia lile likadondoka chini na Mtukufu Mtume[saw] akaliokota na kumuuliza yule adui nani anaweza kukuokoa kwa hili? huku akitetemeka aliomba msamaha na Mtukufu Mtume[saw] akamsamehe na kumuacha aende zake. Na huyo ni adui aliyetaka kutoa maisha yake.

Siku ya ushindi wa Makka haina mfano katika historia ya binadamu. Kwa miaka 13 nyuma Mtukufu Mtume[saw] na masahaba zake walikuwa wameteswa. Waislamu wakawekewa vikwazo vya kutopata chakula baadhi ya masahaba wakahamia Abysinia na Mtukufu Mtume[saw] ikabidi kufanya Hijra ya kwenda Madina na hata huko Madina, Makureish wakaendeleza uhasama, njama na vita. Sasa waislamu walikuwa wameshinda vita na ishara tu kutoka kwa Mtukufu Mtume[saw] ya kuwaua ingetekelezwa kwa haraka. Lakini hakufanya hivyo bali kwa sauti ya upole iliyojaa huruma aliwauliza, ***niambie niwatendee nini?***

Wakionyesha unyenyekevu, aibu na huku wameinamisha vichwa chini walijibu tunatarajia kutoka kwako yale Nabii Yusuph[as] aliyowatendea ndugu zake. Mtukufu Mtume[saw] aliposikia kauli hiyo bila kujali mateso ya nyuma alisema "Nendeni hakuna lawama kwenu Allah Awasamehe kwa hakika yeye ni msamehevu. Nendeni nyote mko huru kwenda.

Kwa matukio haya mawili tunapata Dawa mujarabati ya matatizo tuliyonayo Duniani kwa hivi sasa. Hakuna kosa unaloweza kutendewa na ukakosa kusamehe. Wapo waliofaidika na kujifunza kutoka katika maisha ya Mtukufu mtume Mtukufu Mtume[saw]. Samora Machel, Raisi wa kwanza wa Msumbiji alipigana vita vya msituni na Wareno na vibaraka wao wana Msumbiji. Yalikuwa mauaji makubwa na ukatili, Samora Machel aliwasamehe wote Nchi hiyo ilipojipatia uhuru. Nelson Madiba Mandela miaka 27 alikuwa kwenye kisiwa cha Robben pamoja na Makomredi wenzie. Huku nyuma serikali ya makaburu iliendelea kuwatesa wananchi kupitia sera yao ya ubaguzi wa rangi, mauaji makubwa ya Sharperville na mauaji ya Soweto. Yote haya yalikuwa maumivu makubwa, hata hivyo Nelson Madiba Mandela alitoka jela ukafanyika uchaguzi na akachaguliwa kuwa Rais wa kwanza aliyechaguliwa kidemokrasia na wananchi wa Afrika Kusini siku ya uhuru alitamka yaliyopita si ndwele, tugange yajayo.

Jomo Kenyatta aliyemuomba Sheikh Mubarak Ahmad KITABU cha Maisha ya Muhammad (saw), alipotoka gerezani aliwasamehe wazungu waliomuweka ndani na kumbebesha msalaba wa vita vya Maumau. Alimwahidi Sheikh Mubarak Ahmad ukipatikana uhuru atawasamehe wote. Na kweli alitimiza ahadi yake. Kuinusuru Dunia tuna wajibu wa kusambaza mafundisho aliyoyaleta na kuyaonesha kwa vitendo Mtume Muhammad[saw]. Mafundisho mazuri bila vitendo ni mithili ya jangwa na hakuna kitakachomea.




QUR'AN TUKUFU

Surah 24:34

"Na washike utawa wale wasiopata kuoa mpaka Mwenyezi Mungu Awatajirishe katika fadhili Zake. Na wale wanaotaka hati katika wale inayowamiliki mikono yenu ya kuume, basi waandikieni, kama mkiona wema kwao. Na wapeni katika mali ya Mwenyezi Mungu Aliyowapeni. WALA MSIWASHURUTISHE VIJANA WENU WA KIKE KUFANYA UKAHABA KAMA WAKITAKA KUKAA UTAWANI, ILI KUTAFUTA VIFAA VYA MAISHA YA DUNIA. Na Atakayewashurutisha, basi hakika Mwenyezi Mungu baada ya kushurutishwa kwao ni Msamehevu, Mrehemevu."

وَلْيَسْتَعْفِفِ ٱلَّذِينَ لَا يَجِدُونَ نِكَاحًا حَتَّىٰ {
يُغْنِيَهُمُ ٱللَّهُ مِن فَضْلِهِۦ ۗ وَٱلَّذِينَ يَبْتَغُونَ ٱلْكِتَٰبَ
مِمَّا مَلَكَتْ أَيْمَٰنُكُمْ فَكَاتِبُوهُمْ إِنْ عَلِمْتُمْ فِيهِمْ
خَيْرًا ۖ وَءَاتُوهُم مِّن مَّالِ ٱللَّهِ ٱلَّذِىٓ ءَاتَىٰكُمْ ۚ وَلَا تُكْرِهُوا۟
فَتَيَٰتِكُمْ عَلَى ٱلْبِغَآءِ إِنْ أَرَدْنَ تَحَصُّنًا
لِّتَبْتَغُوا۟ عَرَضَ ٱلْحَيَوٰةِ ٱلدُّنْيَا ۚ وَمَن يُكْرِههُّنَّ فَإِنَّ
ٱللَّهَ مِنۢ بَعْدِ إِكْرَٰهِهِنَّ غَفُورٌ رَّحِيمٌ }

[سُورَةُ النُّورِ: ٣٤]



NUKUU YA HADITHI

Abu Mas'ud Badri[ra] anasimulia ya kuwa: "Mtume (SAW) alihara-misha kutumia mapato yatokanayo na mauzo ya mbwa: NA MAPATO YA MWANAMKE MZINIFU na ada za watabiri na wapiga ramli." **(Bukhari na Muslim)**



Nukuu ya Masih Aliyeahidiwa[as]

Masih Mau'udi a.s anasema: "Njia ya Zinaa ni mbaya sana, yaani INAZUIA KUFIKIA KWENYE LENGO LILILOKUSUDIWA na ni HATARI SANA KWA HATIMA YENU..." (Hekima ya Mafundisho ya Kiislamu, Ruhani Khazain, J. 10, uk.

Imeandaliwa na Musa
Salum 0717504690

Mola wetu,
tumedhulumu nafsi zetu;
na kama Hutusamehe na
kuturehemu, bila shaka
tutakuwa miongoni mwa
wenye hasara. Aamin

BODI YA UHARIRI

Msimamizi:	Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri:	Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta:	Jabiri Faraji Bishazo.
Mchapishaji:	Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji:	Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:	1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
	2. Mahmood Hamsin Mubiru.
	3. Jamil Mwanga.
	4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.

Mjue Jinni

Kutoka Uk 01..

Kwa nini Qur-aan Haimtaji Dajjal?

Wengi huuliza kwa nini Qur-aan inamtaja Yajuj na Maajuj lakini haimtaji Dajjal kwa jina lake. Neno dajjal maana yake mpinga Kristo, au mwongo mkubwa, mlaghai na kafiri, wakati Yajuj na Maajuj ni majina ya mataifa mawili. Vitabu vya hadithi vinatumia neno Dajjal kama neno linalohusisha bishara za Masihi wa siku za mwisho na neno hilo linatuonyesha kwamba linahusu watu wanaosema uwongo na kudanganya na kufanya hivyo katika mambo ya kidini na kidunia. Hivi ndivyo hadithi zinavyomtaja Dajjal kuwa na jicho moja la upofu. Inaonyesha kwamba dajjal atakuwa na jicho litakuwa kipofu kabisa kwenye mambo ya dini. Hata kama Dajjal haja tajwa kwa jina ndani Quran, lakini zimetajwa alama zake kama tulivyo ziona katika sura Khaf.

Hazrat Mirza Ghulam Ahmad a.s anaendelea kusema kuwa:- "Neno Dajjal lina maana mbili: Kwanza, linaashiria kundi linalounga mkono batili na kufanya kazi kwa hila na hadaa. Pili, ni jina la Shetani ambaye ni baba wa wote katika uongo na kuhadaa.

Pia hapa "Dajjal aliyetajwa katika hadithi ameelezewa na Qur'ani Tukufu kama Shetani, ambaye inamnukuu ikisema:-

قَالَ أَنْظِرْنِي إِلَى يَوْمِ يُبْعَثُونَ {7:15} قَالَ {إِنَّكَ مِنَ الْمُنْظَرِينَ 7:16}

Shetani akaomba mbele ya Mwenyezi Mungu apewe muhula mpaka wahuishwe walio kufa. Mwenyezi Mungu akasema: Umepewa muhula mpaka wakati huo.

Hivyo Dajjal ambaye ametajwa katika Hadithi si mwingine ila ni Shetani ambaye atauawa katika siku za mwisho. Haya yameandikwa katika kitabu cha Danieli pia na katika hadithi. Kwa vile Ukristo ndiyo dhihirisho kamili la Shetani, Surah Al-Fatihah haimtaji Dajjal, lakini inaagiza dua ya kimbilio dhidi ya uovu wa Dhwaallin [wale waliopotea] bali imetoa hiyo dua kwa ajili ya usalama dhidi ya Dajjal.

Aya iliyotajwa hapo juu haimaanishi siku ya ufufuo, kwa sababu Shetani ataendelea kuwa hai maadamu tu wanadamu wangali hai. Shetani hafanyi kazi kwa nguvu zake mwenyewe, bali kupitia mawakala wake, ambao ni watu wanaomfanya mwanadamu kuwa mungu. Kwa kuwa ni kundi la watu, wanaitwa Dajjal kama katika Kiarabu Dajjal pia inamaanisha kundi. Iwapo Dajjal atachukuliwa kuwa na maana ya mtu asiyekuwa wahubiri wa Ukristo wapotofu, hii italeta mkanganyiko, kwa sababu hadith zile zile zinazoashiria kwamba Dajjal ataishinda dunia katika siku za mwisho.

Pia hizo hizo hadithi zinaonyesha kwamba katika siku hizo uwezo wa kanisa utazishinda dini zote. Mgongano huu unaweza kutatuliwa tu kwa kuthibitisha kwamba viwili hivyo ni kitu kimoja." (Haqiqat-ul-Wahi, Ruhani Khazain, Juzuu 22, Ukurasa 41).

Dajjal katika Vitabu vya Ahadith

Ni muhimu sana kueleza kwamba Hadithi zinazohusiana na mtazamo wa Dajjal ni nyingi. Na ni wazi kuwa hadithi hutumia maneno ya ndoto au maono wakati wa kuelezea kuonekana kwa Dajjal katika riwaya nyingi sana ambazo Mtukufu Mtume s.a.w alimwelezea Dajjal akisema:-

حَدَّثَنَا إِبْرَاهِيمُ بْنُ الْمُنْذِرِ، حَدَّثَنَا أَبُو ضَمْرَةَ، حَدَّثَنَا مُوسَى، عَنْ نَافِعٍ، قَالَ عَبْدُ اللَّهِ ذَكَرَ النَّبِيُّ صلى الله عليه وسلم يَوْمًا بَيْنَ ظَهْرِي النَّاسِ الْمَسِيحَ الدَّجَّالَ ، فَقَالَ " إِنَّ اللَّهَ لَيْسَ بِأَعْوَرَ، أَلاَ إِنَّ الْمَسِيحَ الدَّجَّالَ أَعْوَرُ الْعَيْنِ الْيُمْنَى ، كَأَنَّ عَيْنَهُ عِنَبَةٌ طَافِيَةٌ ". " وَأَرَانِي اللَّيْلَةَ عِنْدَ الْكَعْبَةِ فِي الْمَنَامِ، فَإِذَا رَجُلٌ آدَمُ كَأَحْسَنِ مَا يُرَى مِنْ أَدَمِ الرِّجَالِ، تَضْرِبُ لِمَّتُهُ بَيْنَ مَنْكِبَيْهِ، رَجِلُ الشَّعَرِ، يَقْطُرُ رَأْسُهُ مَاءً وَاضِعًا يَدَيْهِ عَلَى مَنْكِبَىْ رَجُلَيْنِ وَهُوَ يَطُوفُ بِالْبَيْتِ. فَقُلْتُ مَنْ هَذَا فَقَالُوا هَذَا الْمَسِيحُ ابْنَ مَرْيَمَ ثُمَّ رَأَيْتُ رَجُلاً وَرَاءَهُ جَعْدًا قَطَطًا أَعْوَرَ عَيْنِ الْيُمْنَى كَأَشْبَهِ مَنْ رَأَيْتُ بِابْنِ قَطَنٍ، وَاضِعًا يَدَيْهِ عَلَى مَنْكِبَىْ رَجُلٍ، يَطُوفُ بِالْبَيْتِ، فَقُلْتُ مَنْ هَذَا قَالُوا الْمَسِيحُ الدجال ". تَابَعَهُ عُبَيْدُ اللَّهِ عَنْ نَافِعٍ

Inasimuliwa na Hadhrat Abdullah r.a kuwa Mtume s.a.w alimtaja Masih Dajjal mbele ya watu akisema:

"Mwenyezi Mungu si mwenye jicho moja, na Masih Dajjal ni kipofu wa jicho la kulia na jicho lake linafanana na zabibu zinazo chipuka. Nikiwa nimelala karibu na Ka'ba jana usiku, niliona katika ndoto yangu mwanamume mwenye rangi ya kahawia anayeweza kuonekana vizuri zaidi kati ya rangi ya kahawia na nywele zake zilikuwa ndefu hadi zikaanguka katikati ya mabega yake. Nywele zake zilikuwa duni na maji yalikuwa yakitiririka kutoka kichwani mwake na alikuwa akiweka mikono yake juu ya mabega ya watu wawili huku akiizunguka Ka'ba [yaani akifanya tawafu]. Nikauliza, 'Huyu ni nani?' Wakajibu: Huyu ni Isa bin Mariamu! Nyuma yake nilimuona mtu ambaye alikuwa na nywele zilizopinda sana na alikuwa kipofu wa jicho la kulia, akifanana na Ibn Qatan (yaani kafiri) kwa sura. Alikuwa akiweka mikono yake juu ya mabega ya mtu huku akifanya Tawaf kuzunguka Ka'ba. Nikauliza, 'Huyu ni nani? Wakajibu: Masihi Dajjal. "(Sahih Bukhari, Hadithi namba 3439)

Inafurahisha sana kwamba Mtukufu Mtume s.a.w aliweka wazi kwamba Masihi wa siku za mwisho atakuwa mtu tofauti kabisa na Issa wa awali. Aliona mataifa kuhusiana na maelezo ya Masihi aliyetumwa kwa Bani Israel.

حَدَّثَنَا مُحَمَّدُ بْنُ كَثِيرٍ، أَخْبَرَنَا إِسْرَائِيلُ، أَخْبَرَنَا عُثْمَانَ بْنَ الْمُغِيرَةِ، عَنْ مُجَاهِدٍ، عَنِ ابْنِ عَبَّاس رضى الله عنهما ـ قَالَ قَالَ النَّبِيُّ صلى الله عليه وسلم
رَأَيْتُ عِيسَى وَمُوسَى وَإِبْرَاهِيمَ، فَأَمَّا عِيسَى " فَأَحْمَرُ جَعْدٌ عَرِيضُ الصَّدْرِ، وَأَمَّا مُوسَى فَآدَمُ جَسِيمَ سَبْطُ كَأَنَّهُ مِنْ رِجَالِ الزُّط ".

Imesimuliwa na Hadhrat Ibn Abbas r.a kuwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) amesema: "Nilimwona Musa, Isa na Ibrahimu (usiku wa miraaji) Yesu alikuwa na rangi nyekundu, nywele zilizopinda na kifua kipana, Musa alikuwa na rangi ya kahawia, iliyonyooka, nywele na kimo kirefu kana kwamba anatoka kwa watu wa Az-Zutt." (Bukhari Juzuu ya 5, kitabu cha 55, Hadithi ya 648)

Jambo kuu lililozungumziwa hapa na Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w) aliliona katika hadithi hii ni kwamba ilikuwa ni ndoto. Waislamu wote wanapaswa kufahamu kwamba ndoto hazipaswi kuchukuliwa kidhahiri. Hapa kuna baadhi ya mifano ya wazi kutoka kwenye Qur'an, hadith na wanazuoni wakubwa wa Uislamu. Imeelezwa katika Qur'an:

إِذْ قَالَ يُوسُفُ لِأَبِيهِ يَا أَبَتِ إِنِّي رَأَيْتُ أَحَدَ عَشَرَ كَوْكَبًا وَالشَّمْسَ وَالْقَمَرَ رَأَيْتُهُمْ لِي سَاجِدِينَ {5} قَالَ يَا بُنَيَّ لَا تَقْصُصْ رُؤْيَاكَ عَلَىٰ إِخْوَتِكَ فَيَكِيدُوا لَكَ كَيْدًا إِنَّ الشَّيْطَانَ لِلْإِنْسَانِ عَدُوٌّ مُبِينٌ {6} وَكَذَٰلِكَ يَجْتَبِيكَ رَبُّكَ وَيُعَلِّمُكَ مِن تَأْوِيلِ الْأَحَادِيثِ وَيُتِمُّ نِعْمَتَهُ عَلَيْكَ وَعَلَىٰ آلِ يَعْقُوبَ كَمَا أَتَمَّهَا عَلَىٰ أَبَوَيْكَ مِن قَبْلُ إِبْرَاهِيمَ وَإِسْحَاقَ إِنَّ رَبَّكَ عَلِيمٌ حَكِيمٌ {7

إِذْ قَالَ يُوسُفُ لِأَبِيهِ يَا أَبَتِ إِنِّي رَأَيْتُ أَحَدَ عَشَرَ كَوْكَبًا وَالشَّمْسَ وَالْقَمَرَ رَأَيْتُهُمْ لِي سَاجِدِينَ {5} قَالَ يَا بُنَيَّ لَا تَقْصُصْ رُؤْيَاكَ عَلَىٰ إِخْوَتِكَ فَيَكِيدُوا {لَكَ كَيْدًا إِنَّ الشَّيْطَانَ لِلْإِنْسَانِ عَدُوٌّ مُبِينٌ {6 وَكَذَٰلِكَ يَجْتَبِيكَ رَبُّكَ وَيُعَلِّمُكَ مِن تَأْوِيلِ الْأَحَادِيثِ وَيُتِمُّ نِعْمَتَهُ عَلَيْكَ وَعَلَىٰ آلِ يَعْقُوبَ كَمَا أَتَمَّهَا عَلَىٰ أَبَوَيْكَ مِن قَبْلُ إِبْرَاهِيمَ {وَإِسْحَاقَ إِنَّ رَبَّكَ عَلِيمٌ حَكِيمٌ {7

Kumbukeni siku Yusuf alipomwambia baba yake: Ewe baba yangu! Niliona katika ndoto nyota kumi na moja na jua na mwezi, nikaviona vikinisujudia. Akasema Baba yake Yusuf: Ewe mwanangu kipenzi, usiwasimulie ndugu zako ndoto yako hii, wasije wakakupangia vitimbi juu yako. kwani Shetani ni adui aliye wazi kwa mwanadamu. (Sura ya 12 aya ya 5-7)

Hivyo basi kulingana na maono haya, Yusufu alimwambia baba yake kuhusu ndoto ya nyota kumi na moja na jua na mwezi vikimsujudia. Pia Mwenyezi Mungu Mwenyewe Anasema ndani ya Qur'an:

أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ يَسْجُدُ لَهُ مَنْ فِي السَّمَاوَاتِ وَمَنْ فِي الْأَرْضِ وَالشَّمْسُ وَالْقَمَرُ وَالنُّجُومُ وَالْجِبَالُ وَالشَّجَرُ وَالدَّوَابُّ وَكَثِيرٌ مِنَ النَّاسِ وَكَثِيرٌ حَقَّ عَلَيْهِ الْعَذَابُ وَمَنْ يُهِنِ اللَّهُ فَمَا لَهُ مِنْ مُكْرِمٍ إِنَّ {اللَّهَ يَفْعَلُ مَا يَشَاءُ 2219:}

Je! huoni ya kwamba Allah kinamsujudia kilichomo mbinguni na kilichomo ardhini na jua, na mwezi, na nyota, na milima, na miti, na wanyama, na wengi miongoni mwa watu?

Na wengi imewalazimu adhabu. Na ambaye Allah amemfedhehesha hakuna ampaye heshima. Kwa yakini Allah hufanya apendavyo [22:19]

UK. 04

Mjue Jinni

Kutoka Uk 03..

Sasa ninawauliza wale wasiokuwa Waislamu wa Ahmadiyya kuwa je wanaichukulia ndoto ya Nabii Yusuf kidhahiri? Na yusuf aliisimulia ndoto hii kwa Baba yake tu na Baba yake hakuwa na pingamizi juu ya ndoto hii. Katika Sura hiyo hiyo, Mwenyezi Mungu anatueleza tena kuwa:-

وَدَخَلَ مَعَهُ السِّجْنَ فَتَيَانِ قَالَ أَحَدُهُمَا إِنِّي أَرَانِي أَعْصِرُ خَمْرًا وَقَالَ الْآخَرُ إِنِّي أَرَانِي أَحْمِلُ فَوْقَ رَأْسِي خُبْزًا تَأْكُلُ الطَّيْرُ مِنْهُ نَبِّئْنَا بِتَأْوِيلِهِ إِنَّا نَرَاكَ مِنَ الْمُحْسِنِينَ {37}

Na wakaingia pamoja naye gerezani vijana wawili. Mmoja wao akasema: ' hakika nilijiona katika ndoto nikikamua divai.' Na mwingine akasema, hakika nimejiona katika ndoto, nimebeba mkate juu ya kichwa changu ambao ndege wanaula. Tuambiye hakika yake; kwa hakika sisi tuna kuona u miongoni mwa wafanyao hisani.

Watu hawa wawili wanaomba tafsiri ya ndoto zao kuliko kuzichukulia kidhahiri katika Qur'an. Walikuwa gerezani kwa hivyo ndoto zao zinawezaje kuchukuliwa kidhahiri? Yusuph hakujibu kwa kusema "hapana unadanganya, uko wapi mkate au divai" bali alitafsiri ndoto hizo kwa kusema mmoja wenu ataokoka na mwingine ata uawa na kichwa chake kitaliwa na ndege.

Mwenyezi Mungu pia hakuiacha hivyo hivyo ana tufafanulia zaidi tafsiri hii katika Qur'an na anatuonyesha kwamba ndoto hazipaswi kuchukuliwa kidhahiri.

Mwenyezi Mungu anasema tena katika Sura hiyo hiyo

وَقَالَ الْمَلِكُ إِنِّي أَرَى سَبْعَ بَقَرَاتٍ سِمَانٍ: يَأْكُلُهُنَّ سَبْعٌ عِجَافٌ وَسَبْعَ سُنْبُلَاتٍ خُضْرٍ وَأُخَرَ يَابِسَاتٍ يَا أَيُّهَا الْمَلَأُ أَفْتُونِي فِي رُؤْيَايَ إِنْ كُنْتُمْ لِلرُّؤْيَا تَعْبُرُونَ {44} قَالُوا أَضْغَاثُ أَحْلَامٍ {وَمَا نَحْنُ بِتَأْوِيلِ الْأَحْلَامِ بِعَالِمِينَ {45

Na Mfalme akasema, Nimeona katika ndoto ng'ombe saba wanono, wanakula ng'ombe saba waliokonda, na masuke saba mabichi na mengine saba yaliyokauka. Enyi wakubwa, niagulieni ndoto yangu hii ikiwa ninyi mnaweza kufasiri ndoto. Wakajibu wakisema, 'Ni ndoto zilizo vurugika wala sisi hatujui tafsiri ya ndoto hizi. (Sura ya 12 aya ya 44-45)

Ndoto hizi za mfalme zilifasiriwa na Hadhrat Yusu a.s na zime elezwa kwa kina ndani ya sura ya 12 mnamo elezwa habari za Yusuf. Mwenyezi Mungu pia Alimuonyesha ndoto Mtukufu Mtume s.a.w kuhusiana na Badr. Mwenyezi Mungu Anasema;-

إِذْ يُرِيكَهُمُ اللَّهُ فِي مَنَامِكَ قَلِيلًا وَلَوْ أَرَاكَهُمْ كَثِيرًا لَفَشِلْتُمْ وَلَتَنَازَعْتُمْ فِي الْأَمْرِ وَلَكِنَّ اللَّهَ سَلَّمَ: إِنَّهُ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ {448}

Kumbukeni Mwenyezi Mungu alipokuonyesha katika usingizi wako kwamba wao ni wa chache. Na kama tungali kuonyesha wao ni wengi, mngali tenguka nguvu na mngalizozana sana katika jambo hilo. Lakini Mwenyezi Mungu alilinda. Bila shaka ni mjuzi wa yaliyomo vifuani. [8:44] Kwa hakika Mwenyezi Mungu alimuonyesha Mtume s.a.w kwamba watu walikuwa wachache kwa idadi kuliko walivyokuwa.

Katika Hadith ya Bukhari imeelezwa hivi kwamba;-

حَدَّثَنَا أَبُو الْيَمَانِ، أَخْبَرَنَا شُعَيْبٌ، عَنْ عَبْدِ: اللَّهِ بْنِ أَبِي حُسَيْنٍ، حَدَّثَنَا نَافِعُ بْنُ جُبَيْرٍ، عَنِ ابْنِ عَبَّاس - رضى الله عنهما - قَالَ قَدِمَ مُسَيْلِمَةُ الْكَذَّابُ عَلَى عَهْدِ رَسُول الله صلى الله عليه وسلم فَجَعَلَ يَقُولُ إِنْ جَعَلَ لِي مُحَمَّدُ الأَمْرَ مِنْ بَعْدِهِ تَبِعْتُهُ. وَقَدِمَهَا فِي بَشَرٍ كَثِيرٍ مِنْ قَوْمِهِ، فَأَقْبَلَ إِلَيْهِ رَسُولُ الله صلى الله عليه وسلم وَمَعَهُ ثَابِتُ بْنُ قَيْسِ بْنِ شَمَّاسٍ، وَفِي يَدِ رَسُولِ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم قِطْعَةُ جَرِيدٍ، حَتَّى وَقَفَ عَلَى مُسَيْلِمَةَ فِي أَصْحَابِهِ فَقَالَ " لَوْ سَأَلْتَنِي هَذِهِ الْقِطْعَةَ مَا أَعْطَيْتُكَهَا، وَلَنْ تَعْدُوَ أَمْرَ اللَّهِ فِيكَ، وَلَئِنْ أَدْبَرْتَ لَيَعْقِرَنَّكَ اللهُ ، وَإِنِّي لأَرَاكَ الَّذِي أُرِيتُ فِيكَ مَا رَأَيْتَ ". فَأَخْبَرَنِي أَبُو هُرَيْرَةَ، أَنَّ رَسُولَ اللهِ صلى الله عليه وسلم قَالَ " بَيْنَمَا أَنَا نَائِمٌ رَأَيْتُ فِي يَدَىَّ سِوَارَيْنِ مِنْ ذَهَبٍ، فَأَهَمَّنِي شَأْنُهُمَا، فَأُوحِيَ إِلَيَّ فِي الْمَنَامِ أَنِ انْفُخْهُمَا، فَنَفَخْتُهُمَا فَطَارَا فَأَوَّلْتُهُمَا كَذَّابَيْنِ يَخْرُجَانِ بَعْدِي ". فَكَانَ أَحَدُهُمَا الْعَنَسِي وَالآخَرُ مُسَيْلِمَةَ الْكَذَّابَ .صَاحِبَ الْيَمَامَةِ

Imesimuliwa na Hadhrat Ibn Abbas r.a : "Musailama-al-Kadhdhab (yaani mwongo) alikuja katika zama za uhai wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) akiwa na watu wake wengi (kwenda Madina) na akasema: "Kama Muhammad akinifanya mimi kuwa mrithi wake, nitamfuata. " Mtume (s.a.w) alimwendea pamoja na Thabit bin Qais bin Shams; na Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) alikuwa amebeba kipande cha jani la mtende mkononi mwake kisha Akasimama mbele ya Musailama kadhabu (na maswahaba zake) na akasema: "Hata kama ungeniomba kipande hiki (cha jani), nisingekupa. Huwezi kukwepa hatima yako uliyoandikiwa na Mwenyezi Mungu. Uki ukana Uislamu, Mwenyezi Mungu atakuangamiza. Nafikiri kuwa pengine ni wewe yule yule mtu niliyemwona katika njozi." Abu Huraira aliniambia kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu s.a.w akasema, "Nilipolala, nikaona (katika njozi) bangili mbili za dhahabu zimezunguka mkono wangu, na ilinitia wasiwasi jambo hilo kupita kiasi. Kisha nikaamrishwa na Mwenyezi Mungu katika ndoto yangu, nizipulize na zikapeperukia mbali. Na nikazifasiri zile bangili mbili kuwa ni ishara za waongo wawili watakaotokea baada yangu. (Sahih Bukhari, Juzuu ya 4, Kitabu cha 56, Hadithi namba 817)

Hakuna sahaba yeyote aliyemshutmu Mtume (s.a.w) kwa kuvaa dhahabu. Hivyo kama ndoto hazipaswi kuchukuliwa kidhairi, bali wao walisubiri tafsiri yake. Hawakuanza kumtuhumu Mtume (s.a.w) kuwa kwanini amevaa dhahabu ambayo ni haram katika Uislamu?

Ni dhana ya msingi katika Uislamu kwamba ndoto hufasiriwa, lakini Waislamu wasiokuwa Waahmadiyya kwa masikitiko makubwa wanachukulia kila kitu kuwa ni dhahiri. Kama vile wanavyo sema kuwa atakuja punda mkubwa wa Dajjal atapaa na akipita baharini maji yatafika magotini tu. Ilhali hii ni njozi inatakiwa kufasiriwa ili kupata maana yake haswa.

Njozi ya Hadhrat Imam Abu Hanifa ni kama ifuatavyo:

شعَيْبُ بْنَ أَيُّوبَ الصَّرِيفَينِيُّ ، ثَنَا اَبُو يَحْيَى (حديث مقطوع) ، سَمِعْتُ أَبَا حَنِيفَةَ ، يَقُولُ : " رَأَيْتَ رَوْيَا أَفْزَعَتَنِي ، الْحِمَانِيُّ ، رَأَيْتَ كَأَنِّي أُنْبِشَ قَبْرَ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ ، فَأَتَيْتُ الْبَصرَةَ ، فَأَمَرْتُ رَجُلا يَسأَلَ مُحَمَّدَ بْنَ سِيرِينَ ، فَقَالَ : هَذَا رَجُلٌ يَنْشُرُ أَخْبَارَ الرَّسُول صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ

Shuaib bin Ayyub al-Sarifini amesema ya kwamba, Abu Yahya al-Himmani ametuhadithia, 'Nilimsikia Abu Hanifah akisema, "Niliona ndoto iliyoniogopesha. nilikuja Basrah na nikamuamuru mtu mmoja amuulize Muhammad bin Sirin, akamuuliza, akasema: Mtu huyu atafichua Hadithi za Mtume wa Allah (rehema na amani ziwe juu yake).

Imam Bukhari pia aliona ndoto kama hiyo ambapo alikuwa akiondoa nzi kutoka kwenye mwili wa Mtukufu Mtume s.a.w. Tafsiri ya ndoto hiyo ilikuwa kwamba nzi waliwakilisha Hadith za kutunga na kwamba angeziondoa Hadith hizo na kuzitofautisha na Hadith sahihi.

Hatuzichukulii ndoto za Imam Abu Hanifa na Imam Bukhari Mungu apishe mbali ziwe za kidhahiri, bali zote zilikuwa na tafsiri zake nzuri. Bishara kuhusu siku za mwisho Masihi na Dajjal pia zilikuwa ni njozi na hivyo zinahitaji kufasiriwa. Hii inatuambia kwamba bishara kuhusiana na Dajjal zimejaa usemi wa sitiari [metaphorical] na hazipaswi kuchukuliwa kidhahiri kabisa. Hadithi sahihi zinatuambia kwamba kwa kusoma aya kumi za kwanza na za mwisho za Surah al-Kahf, tutapata ulinzi dhidi ya Dajjal na tayari tumeshaeleza jinsi aya hizi zinavyowataja makasisi wa Kikristo na mafundisho yao ya uwongo wanayoeneza duniani.

Aya kumi za kwanza na za mwisho zote zinatuonya waziwazi kuhusu mataifa ya Kikristo ambayo yanathibitisha zaidi kwamba kwa mujibu wa Qur'an Dajjal mkubwa zaidi ni makasisi wa Kikristo. Kauli nyingine muhimu ya kuzingatia ni hii kwamba kwa mujibu wa hadithi.

ما بين خلق آدم إلى قيام الساعة أمر أكبر من الدجال

Hadithi hii imepokewa kutoka kwa Imran bin Husein (radhi za Allah ziwe juu yake) akisema: Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) akisema: "Baina ya wakati wa kuumbwa kwa Adam na Siku ya Kiyama, hakuna kitu kikubwa zaidi kuliko ubaya wa Dajjal (Mpinga Kristo)." [Muslim] na (Riyad Salihin Kitabu cha 19, Hadith 7)

Ijtimaa ya 34, Khuddam Ahmadiyya Tanzania Yafana.

Ufunguzi wa Ijtmaa ya 34 ya Khuddamul Ahmadiyya Tanzania ulianza kwa upandishwaji wa bendera ambao ulihudhuriwa na Masadr watatu, Sadr wa Khuddamul Ahmadiyya Tanzania Ndugu Rahim Mwanga, Sadr wa Khuddamul Ahmadiyya Kenya Shabir Ombango na Sadr Khudammul Ahmadiyya Uganda ndugu AbdulMalick Ssenfuka. Baada ya hapo ulifuata usomaji wa Quran ukifuatiwa na usomaji wa shairi.



Kisha baada ya hapo ilifuata hotuba ya ufunguzi wa Ijtimaa iliyotolewa na Sadr Khudammul Ahmadiyya Tanzania ambaye aliwahimiza Khuddam katika kujitambua na kulielewa lengo la kuumbwa kwao, Khuddam walihimizwa katika kuitafuta njia ya kweli ya kumwelekea Allah na kujikita katika kuujua umuhimu wa imani zao.

Baada ya hapo mashindano ya kimwili yalianza rasmi kwa mchezo wa mpira wa miguu baina ya Safina Athletics na Central Zone FC ambapo Safina walifanikiwa kuibuka na ushindi na kutinga fainali kwa changamoto ya mikwaju ya penati (4-3).



Ijtmaa ya Majlis Khuddamul Ahmadiyya Tanzania 🇹🇿
Kama ilivyo ada ijtmaa iliambatana na kujitolea damu na usafi wa mazingira, hii ni katika adhma ya khuddam kutimiza wajibu wao wa huduma kwa viumbe.





Akipokelewa Amir na Mbashir Mkuu Jamaat Ahmadiyya Tanzania, Maulana Sheikh Khawaja Muzaffar Ahmad katika Ijtimaa ya 34 ya Khuddam Tanzania.





Bustani ya Washairi

Kun fa yakun

Anapotaka chochote, amuri anaitoa
Mara vinaanza vyote, tii lichoamuria
Hakuna chembe yeyote, inaweza kubishia
Kuni fayakun Amri, kanuni zinafwatia

Huu ulimwengu wote, kwaamuri litokea
Kabla ya nyota yeyote, ratikani vilikua
Fataki lipuka lote, kaiambua Dunia
Kuni fayakun Amri, kanuni zinafwatia

Yakatapakaa kote, matufe yakielea
Dunia Katika yote, uhai ukachipua
Kwahizo hatua zote, zama zilitokomea
Kuni fayakun Amri, kanuni zinafwatia

Kabla mmea wowote, majini walitokea
wakuhitaji chochote, joto Kali walikaa
Maji yalojaa kote, viumbe liibukia
Kuni fayakun Amri, kanuni zinafwatia

Kama mmea wowote, binadamu litokea
Chembe zaaina zote, kwapamoja zilikaa
Miezi mitisa yote, adamu wakaenea
Kuni fayakun Amri, kanuni zinafwatia

Anapoumbwa yeyote, kuwa nayeanakua
Nutifati yeyote, yai kilirutubia
Hatua kipita zote, binadam natimia
Kuni fayakun Amri, kanuni zinafwatia

Kitokeacho chochote, kiumbe kikazaliwa
Kina zipitia zote, hatua lizopangiwa
Hakutowepo chochote, bila ya amuri kuwa
Kuni fayakun Amri, kanuni zinafwatia

Hakutowepo chochote, bila ya amuri kuwa
Anapotaka chochote, maneno ukiambia
Hamaanishi vyovyote, zingaombwe kulizua
Kuni fayakun Amri, kanuni zinafwatia

Hamaanishi vyovyote, zingaombwe kulizua
Bali zile ngazi zote, mpaka kitu kutokea
Muda sisawa Kwa vyote, hulingani hilojua
Kuni fayakun Amri, kanuni zinafwatia

Muda sisawa Kwa vyote, hulingani hilojua
Labda sekunde sipite, au myezi tisa kuwa
Pengine mwaka wote, au Karine potea
Kuni fayakun Amri, kanuni zinafwatia

Pengine mwaka wote, Kwa mungu meshatokea
Anayafahamu yote, kianza mwisho ajua
Kanuni kafuma kote, hataki zivurugua
Kuni fayakun Amri, kanuni zinafwatia

Kanuni kafuma kote, hataki zivurugua
Zunguka sayari zote, ni nyota zazungukiwa
Mashariki siku zote, linako tokea jua
Kuni fayakun Amri, kanuni zinafwatia

Hakuna mtu yeyote, alopata kuzaliwa
Bila ya mbegu zozote, yuterini kutania
Siyesu wala yeyote, kanuni ilitimia
Kuni fayakun Amri, kanuni zinafwatia

Siyesu wala yeyote, kanuni ilitimia
Meri likuwa nazote, yai likarutubia
Ni true hemophradite, mwana akajipatia
Kuni fayakun Amri, kanuni zinafwatia

Ni true hemophradite, mwana akajipatia
Nawengine uwapate, yakubidi jisomea
Mosaicisim yote, nachimerism pia
Kuni fayakun Amri, kanuni zinafwatia

Habadili sikuzote, kanuni lojipangia
Atakufa yeyote, njia asipotumia
Fano asile chochote, robaini kutimia
Kuni fayakun Amri, kanuni zinafwatia

Fano asile chochote, robaini kutimia
Bila kifaa chochote, naangani akapaa
Hatobaki chochote, atashindwa kupumua
Kuni fayakun Amri, kanuni zinafwatia

Hatobaki chochote, atashindwa kupumua
Sipopumua vyovyote, kaboni itamuua
Na atakauka wote, atabaki kuelea
Kuni fayakun Amri, kanuni zinafwatia

Mwenyezi mjuzi yote, hatosema lisokuwa
Namaneno yake yote, yapishani lichokuwa
Zisake maana kote, pale usipoelewa
Kuni fayakun Amri, kanuni zinafwatia

Zisake maana kote, pale usipoelewa
Simkosoe chochote, kwasababu hujajuwa
Yeye ndo mjua yote, nidhambi kumkosowa
Kuni fayakun Amri, kanuni zinafwatia

Masihi omary Stambuli kisagwa

Alubino

Ukatili asilani, alubino kuwauwa
Wanahaki maishani, kuishi kufurahia
Kwani kosa lao nini, paka roho mwawatowa
Tuyapinge mauaji, alubino wateseka

Mwawaumiza kwanini, kipi waliwaibia
Munawatia shidani, viungo kuwanyofoa
Utu wenu siuwoni, huruma kutowajia
Tuyapinge mauaji, alubino wateseka

KWAKHERI ANDANENGA

Nalia nasikitika, Kutwa kucha ninalia,
Machozi yananitoka, Nashindwa kujizuia,
Andanenga kututoka, Katika hii Dunia,
Nalia Mimi nalia, Andanenga kututoka.

Kwahivi ninavyotunga, Ninawahakikishia,
Kanifunza Andanenga, Tisini Asilimia,
Ameondoka Malenga, Wapi nitamalizia,?
Nalia Mimi nalia, Andanenga kututoka.

Ameondoka Fannani, Kwa Mola Katangulia,
Bado Niko Darasani, Somo halijatimia,
Leo Yuko Kaburini, Nikubwa hii Tanzia,
Nalia Mimi nalia, Andanenga kututoka.

Mwalimu wangu Mlezi, Kututoka Naumia,
Kwangu Nikama Mzazi, Nilivyomshuhudia
Kaniongoza Kwa hizi, Njia ninazopitia,
Nalia Mimi nalia, Andanenga kututoka.

Andanenga Vilevile, Kila Nikikumbukia,
Kwakuniamini Yale, Yakwake Kumtunzia,
Tamkumbuka Milele, Mungu akinijalia,
Nalia Mimi nalia, Andanenga kututoka.

Nilipo Kwa Muda huu, Chini Nimejinamia,
Sinyanyui Uso juu, Nafikiri Kwa hisia,
